MAFUNZO YA WALIMU KAZINI NGAZI YA SHULE
KWA MWALIMU WA DARASA LA I-III

Moduli ya Sita:

SAUTI YA HERUFI, JINA LA HERUFI NA SILABI

Mwongozo wa Mratibu wa Mafunzo ya Walimu Kazini Ngazi ya Shule

UKaid
from the British people

equip Tanzania
Education Quality Improvement Programme

Moduli hii imetayarishwa kwa ushirikiano na:

Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi
Ofisi ya Waziri Mkuu – Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa
Taasisi ya Elimu Tanzania
Chuo Kikuu cha Dodoma
Chuo cha Ualimu Morogoro
Chuo Kikuu cha Dar Es Salaam
Chuo Kikuu Huria cha Tanzania
Chuo Kikuu Kishiriki cha Elimu Mkwawa
EQUIP-Tanzania

Moduli hii imewezeshwa kwa ushirikiano na:

C.C.U Butimba
C.C.U Bustani
C.C.U Tabora
C.C.U Ndala
C.C.U Kasulu
C.C.U Kabanga
C.C.U Bunda
C.C.U Tarime
C.C.U Shinyanga
C.C.U Mpwapwa

DIBAJI

Dira ya Maendeleo ya Taifa 2025, imetoa kipaumbele katika sekta ya elimu ili kuleta mageuzi ya kiuchumi na kijamii. Lengo la Dira ya Maendeleo ni kuwa na taifa la watu waliolelimika na jamii iliyo tayari kujifunza kufikia 2025. Serikali ya Tanzania imethibitisha kwa vitendo kuwa Elimu ni kiambato muhimu katika kupunguza umaskini na kuimarisha maendeleo ya taifa. Kwa muda mrefu serikali imetambua kuwa "Ubora wa Elimu yoyote hauwezi kuwa bora kuliko mwalimu mwenyewe" hivyo imetilia mkazo mafunzo kazini kwa walimu kupitia mikakati mbalimbali ili kuimarisha umahiri wa walimu katika ufundishaji na ujifunzaji darasani.

Katika kuongeza ufanisi wa ufundishaji na ujifunzaji darasani, Taasisi ya Elimu Tanzania kwa kushirikiana na EQUIP-Tanzania, wameandaa moduli hii ambayo imesheheni kazi mbalimbali ambazo waalimu mtazitenda katika vikundi wakati wa mafunzo kwa kutumia mbinu ya Mafunzo ya Walimu Kazini ngazi ya shule. Mbinu hii inatambua umuhimu wa walimu kujifunza pamoja na kubaini changamoto zinazowakabili ili kupata suluhisho la changamoto za ufundishaji na ujifunzaji kwa pamoja.

Moduli hii ya Mafunzo ya Walimu Kazini, imeandaliwa ili kusaidia juhudi za Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi kuhakikisha kuwa mbinu fanisi zinatumika darasani wakati wa ufundishaji na ujifunzaji. Moduli hii pia inawasaidia walimu kushirikishana uzoefu na umahiri katika ufundishaji na ujifunzaji darasani. Vilevile Moduli inatoa mafunzo ya ziada ikitarajiwa kuwa walimu watakuwa wamekwisha pata Mafunzo Kabilishi ya utekelezaji wa Mtaala ulioboreshwa wa kuimarisha ufundishaji wa KKK kwa wanafunzi wa darasa la kwanza na la pili.

Taasisi ya Elimu Tanzania inatarajia kuwa moduli hii itawasaidia walimu kuimarisha umahiri wa ufundishaji na ujifunzaji ili kuwasaidia wanafunzi waweze kujenga uwezo unaokusudiwa wakati wa kujifunza.

Changamoto iliyo mbele yetu ni kuhakikisha kuwa tunaonyesha kwa vitendo matokeo mazuri yanayotokana na maudhui ya moduli hii wakati wa ufundishaji na ujifunzaji darasani ili kuimarisha ubora wa elimu ya shule ya msingi.

Dr. Leonard Akwilapo
Kaimu Mkurugenzi Mkuu,
Taasisi ya Elimu Tanzania.

Maelezo Muhimu kwa Mratibu wa Mafunzo ya Walimu Kazini Ngazi ya Shule

Mwongozo huu utatumika sanjari na moduli ya sita ya mwalimu ili kumsaidia mratibu wa mafunzo kuwa na mpangilio mzuri wenye kufuata hatua kwa hatua ili kuwafanya walimu washiriki kikamilifu katika kujifunza maudhui ya moduli ya sita.

Mwongozo huu umegawanyika katika sehemu mbili. Sehemu ya kwanza ambayo ni upande wa kushoto wa mwongozo unabeba maelezo ambayo mratibu wa mafunzo ya walimu kazini ngazi ya shule atatakiwa kuyafuata wakati wa kuratibu kipindi cha kujifunza maudhui ya moduli. Sehemu ya pili ambayo ni upande wa kulia wa mwongozo unabeba maudhui yaliyo kwenye moduli ya mwalimu ambayo watayasoma wakati wa kipindi cha kujifunza.

Wakati wa kipindi cha kujifunza, unatakiwa kufuata maelezo yanayokuongoza yaliyo upande wa kushoto wa mwongozo huu na kuyahusianisha na maudhui yaliyo kwenye moduli ya mwalimu ambayo yapo upande wa kulia wa mwongozo huu kama yanavyosomeka kwenye moduli ya mwalimu.

MAELEKEZO NA TASWIRA KATIKA MODULI

Kuna picha na michoro mingi katika moduli. Baadhi zinajirudia mara nyingi kwa sababu zinamaanisha jambo mahususi linalotokea. Zifuatazo ni mifano ya taswira mbalimbali ambazo zinapatikana katika moduli pamoja na kile ambacho zinawakilisha:

Jadili na mwenzako: Wakati wote wa kusoma moduli, walimu wataelezwa kufanya kazi pamoja na mwalimu mwingine juu ya maswali au kazi.

Fikiri– Wawili wawili – Shirikishana: Kama ilivyo katika maelezo ya hapo juu, hapa vilevile walimu wanafanya kazi wakiwa wawili wawili. Japokuwa, hapa walimu wanatafakari mmoja mmoja kwanza juu ya swali au tatizo, halafu mwalimu anafanya kazi na mwenzake na mwishoni wanawasilisha katika kundi lote.

Jadiliana katika kikundi: Wakati mwingine walimu wataelekezwa kutafakari au kujadili maswali mbalimbali katika kikundi.

Soma: Katika kila moduli kuna "dhana kuu" ambayo kwa kawaida huwasilishwa kwa kirefu katika maelezo.

Andika: Moduli itawahamasisha walimu kuchukua maelezo na kuandika fikra zao na majibu.

Igizo: Baadhi ya mazoezi yatahitaji walimu kuigiza kazi ya kufundisha wakati wengine watapaswa kuigiza kama wanafunzi.

MAELEKEZO KWA MRATIBU WA MAFUNZO KAZINI

Kabla ya kuanza moduli hii, angalia 'maelekezo muhimu' na hakikisha kuwa wewe na walimu mnayazingatia.

Tafadhali waambie walimu wajiorodheshe na kusaini hapo chini.

WAAMBIE WALIMU:

"Sasa tutasoma utangulizi wa moduli hii. Tutasoma matini kwa sauti na kwa kupokezana. Baada ya mwalimu wa kwanza kusoma aya ya kwanza, atamwita mwalimu mwingine kwa jina ili asome aya inayofuata."

Tarehe:	Shule:	Wilaya:	Mkoa:
Muda wa kuanza:	Jina la Mratibu na sahihi yake:		
Muda wa kumaliza:	Jina la Mwalimu Mkuu na sahihi yake:		

	JINA LA MWALIMU	ME / KE	SAHIHI:	DARASA
1				
2				
3				
4				
5				
6				
7				
8				

MODULI YA 6: SAUTI YA HERUFI, JINA LA HERUFI NA SILABI

MAUDHUI YA MODULI

Maudhui ya moduli hii yanahusu dhana kuu tatu za kufundishia kusoma ambazo ni majina ya herufi, sauti za herufi na silabi. Dhana hizi ndiyo msingi wa maneno yanayoandikwa au kutamkwa. Wanafunzi wanapofahamu tofauti kati ya vitu hivi vya msingi na kuvitumia ipasavyo, wanaweza kusoma aina zote za maneno mageni.

DHANA KUU

- **Sauti ya Herufi** – ni kipande kidogo cha sauti ambacho kinawakilisha herufi katika neno linalotamkwa.
- **Jina la Herufi** – Ni kitambulisho kinachoonyesha herufi inavyoweza kutamkwa kwa kuzingatia kanuni zilizokubalika katika kutambua herufi. Mara nyingi hutumia kutamka herufi zinazounda neno.
- **Silabi** – muungano wa sauti ambao kwa kawaida unaundwa kwa kuunganisha konsonanti na irabu.

MALENGO YA MODULI

Mwishoni mwa moduli hii, walimu wataweza:

- Kufahamu tofauti iliyopo kati ya sauti ya herufi, jina la herufi na silabi
- Kufahamu namna ujuzi wa dhana hizi unavyorahisisha mwanafunzi kujua kusoma.
- Kupima ufahamu wa wanafunzi kuhusu sauti ya herufi, jina la herufi na silabi

---

MAELEKEZO MUHIMU

1. Njoo kwenye mafunzo ukiwa na moduli yako ya mafunzo kazini pamoja na kalamu ya wino
2. Unaweza kuja na chakula au kitu cha kutafuna na maji kama mtapanga kukutana mchana baada ya masomo
3. Kifaa chenye maandishi kinachopatikana kwenye mazingira yako kama vile (boksi, gazeti, kitabu, tangazo, kipeperushi, nk.)

TARATIBU ZA KUJIFUNZA KWA KILA KIPINDI

1. Kutana katika sehemu tulivu yenye ubao kama inavyoonekana katika picha
2. Panga madawati/meza ili kuwezesha washiriki wote waonane na kuongea kwa pamoja
3. Kuwa huru kuuliza maswali kama hujaelewa
4. Kuwa wa msaada kwa wenzako
5. Kuwa mbunifu na fikiria jinsi dhana unazojifunza zinahusiana na darasa lako
6. Weka simu yako katika hali ya mtetemo

TAFAKARI

WAAMBIE WALIMU:

“Tangu moduli ya 5, umefanyia mazoezi shughuli mbili kwenye kipindi cha kujifunza kusoma na kuandika. Orodhesha mafanikio uliyoyaona pamoja na changamoto ulizokabiliana nazo wakati wa kufundisha maudhui ya moduli hiyo darasani kwako.

Una dakika 5 kwa ajili ya kazi hii.”

WAAMBIE WALIMU:

“Sasa tutajadili kwa pamoja mafanikio na changamoto katika kikundi.

Kwa kila changamoto ambayo imewasilishwa tufikiri kwa pamoja kuhusu namna ya kukabiliana nayo. Kumbuka kuandika ufumbuzi ambao unaweza kukabiliana na changamoto zilizojitokeza. Tutatumia dakika 10 kwa majadiliano.”

TAFAKARI

Kipindi kilichopita tulijifunza kuhusu **mwalimu kuwasomea kitabu wanafunzi kwa sauti.** Orodhesha mafanikio uliyoyaona pamoja na changamoto ulizokabiliana nazo wakati wa kufundisha maudhui ya moduli hiyo darasani kwako.

ANDIKA PEKE YAKO (DAKIKA 5)
Tafadhali andika kwenye visanduku, mafanikio na changamoto ulizokutana nazo wakati wa kutekeleza mikakati hii katika darasa lako. .

Mafanikio
(Eleza utaratibu uliotumia na fafanua namna ulivyofanikiwa)

Changamoto
(Eleza utaratibu uliotumia na fafanua changamoto zake)

JADILIANA KATIKA KIKUNDI (DAKIKA 10)
- Shirikisha wenzako kwenye kundi, mojawapo ya uzoefu huo.
- Kwa kila changamoto, pendekeza namna ya kukabiliana nayo.
- Wakati wa majadiliano, andika ufumbuzi unaoendana na changamoto ulizozibainisha.

Njia Muhimu za Ufumbuzi
(Mawazo muhimu mahususi kwa wenzetu)

UTANGULIZI

WAAMBIE WALIMU:

"Kama unakumbuka katika Moduli ya 3, tulijifunza juu ya Mchezo wa Kulala. Leo tutacheza mchezo huo katika shughuli yetu ya kupasha joto.

1. Inamisha kichwa juu ya mikono yako ukiwa umefumba macho ili uonekane kama vile umelala. Tafadhali usifumbue macho!
2. Nitasoma maneno mawili na wewe utaamua kama unafikiri maneno hayo yanaanza na sauti inayofanana au inayotofautiana.
3. Kama unafikiri sauti za mwanzo zinafanana, inua mkono wako (ukiwa umeinamisha kichwa kwenye dawati).
4. Kama unafikiri sauti za mwanzo hazifanani, usiinue mkono.

Kwanza tujaribu kwa pamoja mifano michache tukiwa tumefumbua macho. Nitasoma kwa sauti maneno mawili. Kama unafikiri sauti za mwanzo ni zinafanana, inua mkono wako juu. Kama unafikiri sauti za mwanzo hazifanani, usiinue mkono.

(Soma jozi za maneno zifuatazo. Tulia kidogo kati ya kila jozi, pitia jibu sahihi pamoja na walimu).

1. kaka- kata **(jibu sahihi: sauti zinafanana)**
2. kaa – taa **(jibu sahihi: sauti hazifanani)**
3. jiwe – jiko **(jibu sahihi: sauti zinafanana)**
4. baba – saba **(jibu sahihi: sauti hazifanani)**

Sawa, sasa tunacheza Mchezo wa Kulala. Inamisha kichwa juu ya mikono yako ukiwa umefumba macho ili uonekane kama vile umelala. Nitasoma maneno mawili na wewe utaamua kama unafikiri maneno hayo yanaanza na sauti inayofanana au inayotofautiana.

5. bibi – bibo **(jibu sahihi: sauti zinafanana)**
6. jiko – kiko **(jibu sahihi: sauti hazifanani)**
7. paka – taka **(jibu sahihi: sauti hazifanani)**
8. pika – pasi **(jibu sahihi: sauti zinafanana)**
9. bata – baba **(jibu sahihi: sauti zinafanana)**
10. kitu - vitu **(jibu sahihi: sauti hazifanani)**
11. mto – mtu **(jibu sahihi: sauti zinafanana)**
12. maji – nazi **(jibu sahihi: sauti hazifanani)**
13. ali – hali **(jibu sahihi: sauti hazifanani)**

(Baada ya mchezo soma tena jozi ya maneno na toa jibu sahihi kwa walimu).

UTANGULIZI

ZOEZI LA KUCHANGAMSHA (DAKIKA 10)

Kama unakumbuka katika Moduli ya 3, tulijifunza juu ya Mchezo wa Kulala. Leo tutacheza mchezo huu katika kipengele cha kuchemsha bongo shughuli yetu ya kupasha joto.

1. Inamisha kichwa juu ya mikono yako ukiwa umefumba macho ili uonekane kama vile umelala. Tafadhali usifumbue macho!

2. Mratibu wa mafunzo kazini atasoma maneno mawili na wewe utaamua kama unafikiri maneno hayo yanaanza na sauti inayofanana au inayotofautiana.

3. Kama unafikiri sauti za mwanzo zinafanana, inua mkono wako juu (ukiwa umeinamisha kichwa kwenye dawati).

4. Kama unafikiri sauti za mwanzo hazifanani, usiinue mkono.

Kwanza tutajaribu mifano michache kwa pamoja tukiwa tumefumbua macho. Mratibu atasoma maneno mawili na utapaswa kuinua mkono wako kama unafikiri yanaanza na sauti zinazofanana. Usiinue mkono wako kama unafikiri maneno hayo yanaanza na sauti tofauti.

DHANA KUU

WAAMBIE WALIMU:

“Sasa tutasoma maudhui muhimu. Tutasoma matini kwa sauti na kwa kupokezana.

Baada ya mwalimu wa kwanza kusoma sehemu (kwa mfano, aya au maelezo), atamwita mwalimu mwingine kwa jina ili asome sehemu inayofuata.

Wakati wa kusoma weka alama zifuatazo kwenye matini unayosoma.

Weka alama ya mshangao (!) Kwenye wazo ambalo unadhani ni muhimu.

Weka alama ya kuuliza (?) Kuonesha kutokukubaliana na dhana hiyo.

Weka alama ya duara (O) kuonesha kuwa dhana hiyo ni mpya kwako.”

DHANA KUU

SAUTI YA HERUFI, JINA LA HERUFI NA SILABI (DAKIKA 40)

1. Mwalimu mmoja aanze kusoma kwa sauti. Baada ya kukamilisha sehemu (kwa mfano, aya au maelezo) amwite mwalimu mwingine kwa jina asome sehemu inayofuata.
2. Wakati unaposoma zingatia alama zifuatazo:
    - Weka alama ya mshangao (!) katika sehemu ambayo unaona ni muhimu
    - Weka alama ya kuuliza (?) katika sehemu ambayo huelewi au hukubaliani nayo
    - Weka mduara katika (o) maneno ambayo ni mapya.

Kujifunza kusoma kunaanza kwa kusikia na kutambua sauti. Wanafunzi wengi wanaanza shule wakiwa tayari wanaweza kuzungumza lugha (Kiswahili au lugha ya mama au zote kwa pamoja). Ili waweze kusoma maneno yaliyoandikwa ya Kiswahili, wanahitaji kuwa na ujuzi wa kuhusianisha sauti wanazozisikia katika lugha wanayozungumza, na alama za maandishi wanazoziona. Kwa mantiki hii, Kujifunza kusoma kunaanza kwa mwanafunzi kutambua kuwa:

Moduli hii inalenga hatua ya kwanza – kuwasaidia walimu kusikia na kutofautisha sauti katika maneno ya Kiswahili. Vipande hivi vidogo vya sauti huitwa **Sauti za Herufi.** Sauti ya herufi ni moja ya dhana tatu za msingi ambazo zinaweza kuwasaidia wanafunzi kujifunza kusoma na kuandika maneno:

1. **Sauti ya Herufi:** wanafunzi wanapofahamu sauti za herufi na kuzihusianisha na herufi zilizoandikwa, wanaweza sasa kuanza kutamka (kufichua) maneno mageni yaliyoandikwa.
2. **Jina la Herufi:** wanafunzi wanaweza kutumia jina la herufi wanapo jaribu kutamka herufi zinazounda neno linalotamkwa au kuandikwa.
3. **Silabi:** kama wanafunzi wanaweza kutambua silabi kwa haraka, basi wanaweza kuunda maneno kwa kuunganisha silabi katika maneno marefu na mageni kwao.

Mara tu wanafunzi wanapoweza kutambua na kutumia vitu hivi vitatu muhimu, wanaweza kusoma aina zote za maneno bila kujali ni mapya au la!

DHANA KUU

(Sisitiza maelekezo kwa kuwaambia walimu wawageukie wenzao na kutazama midomo inavyobadilika wanaposema 'maji' taratibu sana).

(Hakikisha kwamba mwalimu anatamka 'ma' taratibu sana).

DHANA KUU

SAUTI YA HERUFI

Sauti ya herufi ni kile kipande kidogo cha sauti kinachosikika mwanzoni mwa kila neno linalotamkwa au kusomwa. Wakati wa chemsha bongo tulijifunza mifano ya maneno ambayo yana sauti zinazotofautiana kwasababu yanaanza na sauti tofauti za herufi, kama vile 'maji' na 'nazi'. Unapotamka haya maneno unasema sauti tofauti za herufi 'm' na 'n'.

Tamka neno 'maji' taratibu sana: /mmm/ /aaa/ /jjj/ /iii/

/mmm/

/aaa/

/jjj/

/iii/

Wakati wa kutamka sauti zinazounda neno hili zingatia zaidi namna midomo yako na ulimi vinavyobadilika unapotamka sauti mbalimbali. Mabadiliko haya yanaonesha kwamba unatamka sauti za herufi tofauti. Mgeukie mwenzako na uangalie midomo yake inavyobadilika akisema 'maji' taratibu.

Ni muhimu kukumbuka kwamba kila herufi ina sauti yake yenyewe. Uliposema 'maji' taratibu, ulikuwa ukiunganisha hizi sauti moja moja kwa pamoja. Mfano,

Tamka 'ma' taratibu sana: /mmm/ /aaa/

/mmm/

/aaa/

Ulipoanza kusema hivi, midomo yako ilikuwa imeshikamana pamoja ili kutengeneza sauti ya /mmm/. Kisha mdomo wako ukafunguka ili kutamka sauti /aaa/. Hii inaonesha kwamba 'm' na 'a' zina sauti mbili zinazotofautiana. Mgeukie mwenzako na uangalie midomo yake inavyobadilika anapotamka 'ma' taratibu sana.

Kama bado huna uhakika na sauti ya herufi 'm', namna ingine ya kuitambua ni kutenga, 'mti' au 'mkate'. Matamshi ya maneno haya yanatenga yenyewe **sauti ya herufi** hiyo moja kwa moja.

DHANA KUU

(Hakikisha kwamba mwalimu anatamka 'mti' taratibu sana).

(Hakikisha kwamba mwalimu anatamka fa, fe, fi, fo, fu taratibu sana).

DHANA KUU

Tamka neno 'mti' taratibu <u>sana</u>: /mmm/ /ttt/ /iii/

/mmm/

/ttt/

/iii/

Ulipoanza kusema hivi, midomo yako ilikuwa imegandamizwa pamoja ili kutengeneza sauti /mmm/. Kisha mdomo wako ukafunguka na ulimi ukagusa sehemu ya juu ya mdomo ili kutengeneza sauti /ttt/. Hii ndiyo tofauti iliyo dhahiri zaidi katika sauti ya herufi kwasababu ni ngumu zaidi kuunganisha sauti /m/ na /t/.

Ni muhimu kutambua na kutenga sauti za kila herufi katika alfabeti. Wanafunzi wanapofahamu sauti za herufi na wakaweza kuzihusianisha na herufi zilizoandikwa, sasa wanaweza kuanza kutamka (kufichua) maneno mageni yaliyoandikwa.

Si rahisi kubaini sauti za herufi za konsonanti za Kiswahili kwa sababu walimu wamezoea kufundisha jina la herufi ambalo hutamkwa kama silabi inayoundwa kwa kuunganisha konsonanti na irabu wakati muunganiko huo wa sauti mbili huwakilisha herufi moja. Hata hivyo, ni muhimu sana kufahamu kwamba **<u>kila herufi ina sauti yake ya kipekee</u>.** Kwa mfano,

Tamka 'fa', 'fe', 'fi', 'fo', 'fu' taratibu <u>sana</u>:

/fff/ /aaa/

/fff/ /eee/

/fff/ /iii/

/fff/ /ooo/

/fff/ /uuu/

Ni sauti ipi ambayo unaisiki katika silabi zote? Unaweza kutamka sauti ya herufi /f/ kwa kuuma mdomo uliogikunja na meno ya juu huku ukipuliza hewa kwenda nje.

Sasa tamka silabi zifuatazo taratibu: ***sa se si so su***
Je, ni sauti gani umeisikia ikijirudia? Sauti iliyokuwa ikijirudia ni sauti ya herufi 's'.

Kama unavyoweza kuona, sauti ya herufi uliyoibaini hivi punde ni tofauti sana na namna unavyoitamka. Hii ndiyo tofauti kati ya **sauti** ya herufi na **jina** la herufi.

Kuna vitu viwili muhimu vya kukumbuka kuhusu sauti za herufi. Kwanza, baadhi ya sauti za herufi ni rahisi kuzitoa kuliko zingine. Hii ni kwa sababu sauti zingine ni rahisi kuzitoa kwa muda wa sekunde kadhaa. Kwa mfano, /sss/ na /mmm/ ni sauti ambazo unaweza kuzitoa kwa muda wa sekunde 2-3. Sauti za herufi ambazo ni ngumu zaidi kuzitoa ni zile ambazo zina sauti fupi. Mfano, /b/ na /t/ ni sauti ambazo zinaweza kutolewa tu kwa haraka. Ni kama vile ukipiga makofi-huwezi kufanya sauti ikadumu kwa sekunde 2-3. Wakati mwingine, njia rahisi ya kutoa sauti fupi ni kuzitoa kwa haraka na kimya, kama vile unanong'ona.

DHANA KUU

WAAMBIE WALIMU:

“ Tunaendelea kusoma matini kwa sauti na kwa kupokezana.”

DHANA KUU

SAUTI NDEFU ZA HERUFI	SAUTI FUPI ZA HERUFI
/f/, /h/, /l/, /m/, /n/, /r/, /s/, /v/, /z/ Na irabu : /a/, /e/, /i/, /o/, /u/	/b/, /ch/, /d/, /g/, /j/, /k/, /p/, /t/, /w/, /y/

Jambo la pili kukumbuka kuhusu sauti za herufi ni kuhusu namna ya kuzirejea katika maandishi. Mwanzoni mwa moduli hii sauti za herufu ziliandikwa hivi : /sss/ na /mmm/.

Hii ilifanyika kuweka mkazo kwamba unapaswa kutamka sauti za herufi polepole sana. Hata hivyo, katika hali halisi, sauti za herufi zinaandikwa kama unavyoziona katika visanduku vilivyopo hapo juu : /s/ na /m/. Kuna herufi moja tu iliyoandikwa katikati ya vipande vya mistari mshazari. Hii ni tofauti na unavyoandika jina la herufi ambalo linaandikwa kwa kutumia alama za kufunga na kufungua : 's' na 'm'.

JINA LA HERUFI

Uzoefu unaonesha kuwa walimu wengi wanaofundisha lugha ya Kiswahili hutumia alfabeti za Kingereza wanapofundisha alfabeti ya Kiswahili. Lakini majina ya herufi za Kiswahili ni tofauti sana na majina ya herufi za Kiingereza. Majina ya herufi za Kiswahili yanakuwa kama vile yameundwa kwa kuongeza 'e' katika konsonati. Mfano : be, che, de, fe. Hata hivyo, majina ya herufi za irabu yanafanana na sauti za herufi zake : a, e, i, o, u.

Kwa hiyo, ni lazima kutamka herufi za Kiswahili kama hivi:
a, be, che, de, e, fe, ge, he, i, je, ke, le, me, ne, o, pe, re, se, te, u, ve, we, ye, ze

Ni muhimu kukumbuka kwamba, sauti ya herufi ni tofauti na **jina la herufi.** Jina la herufi ni kanuni iliyokubalika ya kuitambua herufi husika na hutumika wakati wa kutaja herufi zinaounda neno. Vile vile ni muhimu kukumbuka kwamba, kama unaandika jina la herufi tumia funga na fungua semi (' ').

Tamka herufi za alfabeti hizi: 'm' 'f' 's'

Utagundua kwamba umetamka herufi 'm' ambayo ukitamka utasikia sauti /me/ na herufi 'm' huunda sauti /m/. Hali kadhalika kwa herufi 'f' na 's' ambazo ukizitamka utasikia sauti 'fe' na 'se' ambazo huunda sauti /f/ na /s/. Maneno **pekee** katika alfabeti ya Kiswahili ambayo sauti ya herufi na jina la sauti vinafanana ni irabu: ***a, e, i, o, u.***

DHANA KUU

WAAMBIE WALIMU:

“Ukiwa na mwenzako, fanyeni zoezi la kutambua tofauti kati ya sauti za herufi na majina ya herufi. Angalia neno la kwanza na ulitamke taratibu sana, tambua sauti ya herufi na kisha useme jina la herufi hiyo. Kila mtu afanye zoezi kwa kutumia maneno manne. Kisha shirikisheni majibu yenu kwenye kikundi. Kama kuna mwalimu atakakosa mshirika mwenzake, mratibu a tashirikiana na mwalimu huyo.”

Majibu sahihi:

1. ndiyo
2. ndiyo
3. ndiyo
4. hapana
5. ndiyo
6. ndiyo
7. ndiyo
8. hapana

DHANA KUU

Hebu tujaribu mfano mwingine:

Tamka neno 'watu' taratibu sana: /w/ /a/ /t/ /u/

Ulipoanza kutamka /w/, midomo yako ilijivuta kwa juu huku mashavu yakiingia kwa ndani na kisha midomo kufunguka haraka kutengeneza sauti ya /w/. Kisha mdomo wako ukafunguka ili kutengeneza sauti ya /a/. Sauti ya herufi ya kwanza /w/ ni tofauti sana na jina lake la herufi, ambalo ni 'w' ila ukitamka unasikia sauti 'we' linasikika kama vile 'we'. Lakini sauti /a/ inasikika kama jina lake kwasababu ni irabu.

Ni jambo zuri kufahamu kuwa sauti ya herufi unaweza kuisikiliza vizuri kama utatamka neno taratibu wakati jina la herufi hutamkwa kama silabi ambayo imeundwa kutokana na konsonanti na irabu 'e'. Kwa mfano ukitamka neno 'mama' taratibu utasikia sauti /m/ /a/ /m/ /a/. Sauti /m/ unaweza kuisikia pia unapotamka sauti ya mwanzo ya neno 'mti'. Tofauti na sauti ya herufi, jina la herufi 'm' hutamkwa 'me' kama sauti ya silabi lakini huandikwa 'm'.

FIKIRI - WAWILI WAWILI - SHIRIKISHANA (DAKIKA 10)

Ukiwa na mwenzako, fanyeni zoezi la kutambua tofauti kati ya sauti za herufi na majina ya herufi. Angalia neno la kwanza na ulitamke taratibu sana, bainisha jina la herufi kwanza kisha ubainishe sauti inayounda herufi husika. Kila mtu afanye zoezi la maneno manne. Kisha shirikisheni majibu yenu kwenye kikundi. Kama kuna mwalimu atakaye kosa mshiri ka katika zoezi, mratibu atashirikiana na mwalimu huyo.

Tamka neno hili taratibu sana	Tambua sauti ya herufi	Sema jina la herufi	Je, sauti ya herufi na jina la herufi ni tofauti?
1. yake	/y/	'y'	
2. tatu	/t/	't'	
3. baba	/b/	'b'	
4. andazi	/a/	'a'	
5. lima	/l/	'l'	
6. hapa	/h/	'h'	
7. kaka	/k/	'k'	
8. uhuru	/u/	'u'	

DHANA KUU

WAAMBIE WALIMU:

“ Tunaendelea kusoma matini kwa sauti na kwa kupokezana.”

DHANA KUU

SILABI

Silabi ni muungano wa sauti ambao kwa kawaida unaundwa kwa kuunganisha konsonanti na irabu, kama vile 'da'. Silabi kama hii imeundwa na sauti mbili za herufi za: /d/ + /a/ = da

Tamka: *da de di do du*

Kikanuni, silabi hizi zimeundwa kwa kuunganisha sauti /d/ na sauti /a/ /e/ /i/ /o/ /u/

Silabi inaweza pia kuundwa na irabu peke yake. Kwa mfano, neno "ua" lina silabi mbili: "u" na "a". Neno hili pia lina sauti mbili za herufi: /u/ + /a/ = ua.

Kipekee, konsonanti 'm' na 'n' zenyewe zina sifa ya pekee kwani zinapofuatana na konsonanti hubadilika kuwa silabi badala ya sauti ya herufi. Mfano neno 'mti' ukitenganisha utapata silabi mbili ambazo ni /m/ + /ti/ hali kadhalika neno 'nje' ukilitenganisha utapata silabi mbili ambazo ni /n/+ je/. Kwa upande mwingine neno 'mti' limeundwa na sauti tatu za herufi ambazo ni /m/ + /t/ + /i/ pia neno 'nje' limeundwa na sauti tatu za herufi ambazo ni /n/ + /j/ + /e/

Kama wanafunzi wanaweza kutambua silabi kwa haraka, wananaweza kutenga maneno mageni na yaliyoundwa na silabi nyingi katika vipande hivi vidogo vidogo. Kutenga silabi katika sauti za herufi kunawawezesha wanafunzi kufichua maneno mageni au yasiyotumika mara kwa mara.

MIKAKATI YA KUFUNDISHA SAUTI YA HERUFI, JINA LA HERUFI NA SILABI

Sasa kwa kuwa tuna uelewa mzuri zaidi wa tofauti kati ya hizi dhana tatu, ni muhimu kukumbuka njia mbalimbali za kufundisha wanafunzi kujifunza kusoma kwa kutumia kila dhana kwa usahihi.

Sauti ya herufi:

Njia rahisi inayosaidia kufundisha na kuonesha kwa vitendo sauti za herufi ni kutumia mkakati wa 'Ninafanya-Tunafanya-Mnafanya'. Mfano:

Onesho la Mwalimu 'Ninafanya'	Mwalimu na Wanafunzi 'Tunafanya'	Wanafunzi 'Mnafanya'
1. Tamka neno 'sita' taratibu sana. Waoneshe wanafunzi jinsi ya kusema neno taratibu sana.	2. Tamka 'sita' taratibu sana pamoja na wanafunzi. Waambie wawe makini kuangalia jinsi midomo na ulimi wao unavyobadilika jinsi wanavyotamka sauti tofauti za herufi. Wakati mdomo unabadilika, wanatengeneza sauti tofauti za herufi.	3. Waambie wanafunzi waseme wao wenyewe 'sita' taratibu. Kisha waulize, 'Mnasikia sauti gani mwanzoni mwa neno sita? Darasa linatakiwa kujibu: /s/

Fanya zoezi la kutambua sauti ya herufi kama hiyo katika maneno tofauti (kwa mfano, sasa, soko, sema). Hii inawasaidia wanafunzi kusikia sauti hizo katika muktadha mbalimbali.

DHANA KUU

WAAMBIE WALIMU:

“ Tunaendelea kusoma matini kwa sauti na kwa kupokezana.”

DHANA KUU

Jina la herufi:
Unaweza vile vile kutumia mkakati wa 'Ninafanya-Tunafanya-Mnafanya' kufundisha majina ya herufi. Mfano:

Onesho la Mwalimu 'Ninafanya'	Mwalimu na Wanafunzi 'Tunafanya'	Wanafunzi 'Mnafanya'
1. Andika ubaoni herufi ya 's'. Tamka 'se' na eleza kwamba hili ni jina la herufi la kiwakilishi hiki.	2. Onesha herufi katika ubao na tamka 'se' pamoja na wanafunzi. Weka msisitizo katika kutamka herufi.	3. Sasa onesha herufi ubaoni na uwaulize wanafunzi waseme jina la herufi wao wenyewe, Kisha waulize, 'Nini jina la herufi la kiwakilishi hiki?' Darasa linapaswa kujibu: 'se'

Kuna njia nyingi za kufundisha wanafunzi kukumbuka jina la herufi. Katika moduli ya 1, tulijadili mikakati ya 'herufi ya siku' na 'wimbo wa alfabeti'. Hakikisha kwamba wanafunzi wanafahamu kwamba jina la herufi ni tofauti na sauti ya herufi.

Katika moduli ya 8, tutajadili mkakatika unaofaa ambao unaitwa 'jina – neno kuu – sauti'. Mkakati huu utakusaidia kufundisha majina ya herufi na sauti za herufi kwa mara moja.

Silabi:
1. Mara nyingi walimu wengi hufundisha kujifunza kusoma kwa kuanza na irabu, kisha hufundisha konsonanti ili mwanafunzi anapounganisha konsonanti na irabu aweze kupata sauti moja mbayo hujulikana kama silabi. Njia hii ina tija lakini pia inasaidia sana kuonesha kwamba kila silabi imeundwa na sauti mbili za herufi (pa = /p/ + /a/)
2. Ni muhimu pia kuonesha kwamba, kuunganisha silabi mbalimbali kwa pamoja kunasaidia kuunda maneno mapya. (kwa mfano, unaweza kutumia "pa" katika neno "paka" pia katika neno "pata").
3. Tutajadiliana mikakati mingine zaidi juu ya kufundisha silabi katika moduli ya 8 na 9.

Angalizo: Mwalimu awe makini kutofautisha jina la herufi na sauti ya herufi kwa kuwa mara nyingi wanafunzi hujifunza jina la herufi huku wakitamka silabi, mfano herufi 'b' hutamkwa 'be' na anapofundisha silabi wanafunzi wanapata tabu kuelewa kwa kuwa jina la herufi na silabi hutamkwa sawasawa. Mfano, anapofundisha jina la herufi 'b' wanafunzi hutamka 'be' na anapofundisha 'ba' wanafunzi hutamka 'bea' kutokana na maelekezo ya awali ambayo walijifunza kuwa herufi 'b' hutamkwa 'be'.

DHANA KUU

WAAMBIE WALIMU:

“Sasa kila mwalimu anaweza kuwashirikisha wengine, kitu ambacho ameona ni muhimu, hakieleweki au ni kipya. Kisha tunaweza kujadili namna sauti ya herufi, jina la herufi na silabi vinavyoweza kusaidia wanafunzi kusoma na kuandika.”

Jibu namba 4:

1. **Sauti ya herufi:** wanafunzi wanapofahamu sauti za herufi na kuzihusianisha na herufi zilizoandikwa, ndipo wanaweza kusoma (kusoma kwa sauti) maneno mageni yaliyoandikwa.

2. **Jina la herufi:** wanafunzi wanaweza kutumia majina ya sauti wanapojaribu kutaja herufi za neno lililozungumzwa.

3. **Silabi:** Kama wanafunzi wanaweza kutambua silabi kwa haraka, ndipo sasa wanaweza kutenga maneno wanayoyajua na wasiyoyajua katika hivi vipande vidogo vidogo.

DHANA KUU

JADILIANA KATIKA KUNDI KUBWA (DAKIKA 10)

1. Ni dhana ipi muhimu uliyoweka alama ya mshangao (!)?
2. Ni dhana ipi ambayo haieleweki uliyoiwekea alama ya kuuliza (?)?
3. Ni dhana ipi mpya uliyoizungushia duara?
4. Unadhani kujua sauti za herufi, majina ya herufi na silabi kunaweza kuwasaidia wanafunzi kusoma na kuandika maneno?

VITENDO

WAAMBIE WALIMU:

"Ili kufundisha sauti za herufi, majina ya herufi na silabi kwa ufanisi, ni muhimu walimu wawe na ufahamu mkubwa wa kila kimoja kati ya vitu hivi vitatu. Kazi zifuatazo zitakupa fursa ya kufanya zoezi la kutambua na kutumia kila dhana."

KAZI YA KWANZA – Sasa nitasoma maneno kadhaa. Kwa kila neno nitakalotamka, andika sauti ya herufi ya kwanza unayoisikia. Kwa mfano, nitatamka neno 'soma' kisha unaandika sauti ya herufi ya mwanzo (sio neno). Kisha nitakuambia useme sauti inayoundwa na herufi hiyo kwa sauti.

1. **andazi** (jibu sahihi: /a/)
2. **embe** (jibu sahihi: /e/)
3. **nazi** (jibu sahihi: /n/)
4. **tano** (jibu sahihi: /t/)
5. **bata** (jibu sahihi: /b/)

(Mnaweza kupitia majibu kwa pamoja mtakapokuwa mmemaliza)

KAZI YA PILI – Sasa nitasoma maneno mengine lakini safari hii utaandika sauti ya herufi ya mwisho unayoisikia. Kwa mfano, nitasema: muziki, kisha wewe unaandika sauti ya herufi ya mwisho (sio neno). Kisha nitakuambia useme sauti ya herufi hiyo kwa sauti.

1. **jiko - /o/**
2. **karanga - /a/**
3. **chumvi - /i/**
4. **dume - /e/**
5. **fahamu - /u/**

(Mnaweza kupitia majibu kwa pamoja mtakapokuwa mmemaliza)

VITENDO

ZOEZI (DAKIKA 40)
Ili kufundisha sauti za herufi, majina ya herufi na silabi kwa ufanisi, ni muhimu walimu wawe na ufahamu wa kutosha wa dhana hizi tatu. Kazi zifuatazo zitakupa fursa ya kufanya zoezi la kutambua na kutumia kila dhana.

KAZI YA KWANZA: SAUTI YA MWANZO YA HERUFI

Mratibu wa mafunzo kazini atasoma maneno kadhaa. Kila neno linalotamkwa, andika **sauti ya herufi unayoisikia mwanzo wa kila neno** (usiandike neno). Baada ya kuandika sauti ya herufi, mratibu atamwambia kila mwalimu atamke hiyo **sauti ya herufi** kwa sauti.

Mfano:
Mratibu atatamka neno soma
Unaandika /s/ na kutamka sauti ya herufi hiyo kwa sauti kuwa ni /s/

1. _____
2. _____
3. _____
4. _____
5. _____

KAZI YA PILI: SAUTI YA MWISHO YA HERUFI

Sasa MRATIBU WA MAFUNZO KAZINI atasoma maneno mengine lakini safari hii utaandika sauti ya herufi ya mwisho unayoisikia. Baada ya kuandika **sauti ya herufi** hiyo, MRATIBU atamwambia kila mwalimu aseme **sauti ya herufi** hiyo kwa sauti.

Mfano:
Mratibu atatamka neno rafiki
Unaandika /i/ na kutamka sauti ya herufi hiyo sauti kuwa ni /i/

1. _____
2. _____
3. _____
4. _____
5. _____

VITENDO

KAZI YA TATU – Sasa nitasoma maneno yasiyo kuwa na maana. Andika sauti ya herufi ya kwanza unayoisikia. Kwa mfano, nitatamka neno 'musatimi', kisha unaandika sauti ya herufi ya mwanzo (sio neno). Kisha nitakuambia useme sauti inayoundwa na herufi hiyo kwa sauti.

1. **wuzi**
2. **hameno**
3. **pumeka**
4. **oliotami**
5. **bustafiko**

(Mnaweza kupitia majibu kwa pamoja mtakapokuwa mmemaliza)

KAZI YA NNE – Sasa angalia herufi zilizomo kwenye kisanduku. Katika kikundi, tutasoma kwa pamoja majina ya herufi kwa sauti. Kisha, tutazungushia duara herufi zile ambazo jina la herufi linafanana na sauti ya herufi.

(Majibu: i , A, E, u, o)

VITENDO

KAZI YA TATU: SAUTI YA MWANZO YA MANENO YASIYO KUWA NA MAANA

Sasa mratibu wa mafunzo kazini atasoma maneno kadhaa yasiyo kuwa na maana. Kila neno linalotamkwa, andika **sauti ya herufi unayoisikia mwanzo wa kila neno** (usiandike neno wala herufi). Baada ya kuandika sauti ya herufi, mratibu atamwambia kila mwalimu atamke hiyo **sauti inayoundwa na herufi** kwa sauti.

Mfano:
Mratibu anasema: musatimi
Unaandika /m/ na kutamka sauti ya herufi hiyo sauti kuwa ni /m/

1. _____
2. _____
3. _____
4. _____
5. _____

KAZI YA NNE: BAINISHA HERUFI

Angalia herufi zilizomo katika kisanduku hapa chini. Katika kikundi, soma kwa pamoja majina ya herufi kwa sauti na sauti ya herufi. Kisha, zungushia duara herufi zile ambazo **majina ya herufi** yanafanana na **sauti za herufi.**

(Dokezo: kama hujaelewa vizuri dhana ya jina la herufi, angalia maelezo ya jina la herufi katika Dhana Kuu)

s	**V**	**w**	**i**
A	**h**	**E**	**B**
p	**R**	**z**	**u**
o	**m**	**g**	**K**

VITENDO

KAZI YA TANO – Tazama kwa uangalifu katika maandishi uliyoleta leo, ukisoma kila neno na kuhesabu silabi. Kisha andika maneno mawili kwa kila safu katika jedwali hapa chini.

WAAMBIE WALIMU:

"Sasa kwa kuwa tumemaliza mazoezi, hebu tujibu maswali haya ya mjadala kwa kuzungumza tu. Hakuna haja ya kuandika, changia tu mawazo yako katika kikundi kwa kuzungumza."

Jibu namba 1: Kazi ya 1, 2, 3 zilijielekeza katika sauti za herufi, kazi ya 4 ililenga majina ya herufi na shughuli namba 5 ililenga silabi.

Jibu namba 3: **Sauti ya Herufi:** wanafunzi wanapofahamu sauti za herufi na kuzihusianisha na herufi zilizoandikwa, ndipo wanaweza kuanza kutamka (kusoma kwa sauti) maneno mageni yaliyoandikwa.

Jina la Herufi: wanafunzi wanaweza kutumia jina la herufi wanapojaribu kutamka herufi za neno (kutaja herufi) lililozungumzwa.

Silabi: kama wanafunzi wanaweza kutambua silabi kwa haraka, wanaweza pia kutenga maneno marefu na mageni katika vipande hivi vidogo vidogo vya sauti.

VITENDO

KAZI YA TANO: KUHESABU SILABI

Angalia kwa uangalifu maandishi uliyoleta leo, ukisoma kila neno na kuhesabu silabi. Kisha, andika maneno 2 kwa kila safu katika jedwali lifuatalo.

Maneno yanayoundwa na Silabi Mbili	Maneno yanayoundwa na Silabi Tatu	Maneno yanayoundwa na Silabi Nne	Maneno yanayoundwa na Silabi Tano

JADILIANA KATIKA KUNDI KUBWA (DAKIKA 10)

1. Ni kazi zipi zililenga zaidi kwenye sauti ya herufi? Jina la herufi? na Silabi?
2. Ni kazi zipi zilikuwa changamoto wakati wa kujadiliana? Kwanini unafikiri ilikuwa hivyo?
3. Je, ni kwa namna gani unaweza kutofautisha sauti ya herufi, jina la herufi na silabi?
4. Je, ni kwa namna gani dhana hizi tatu (sauti ya herufi, jina la herufi na silabi) zinasaidia kukuza uwezo wa kujifunza kusoma?

KUPANGA MKAKATI

WAAMBIE WALIMU:

“Sasa tutasoma kuhusu kuandaa kipindi cha kusoma na kuandika. Tutasoma matini kwa sauti na kwa kupokezana.

Baada ya mwalimu wa kwanza kusoma sehemu (kwa mfano, aya au maelezo), atamwita mwalimu mwingine kwa jina ili asome aya inayofuata. “

KUPANGA MKAKATI

KUANDAA 'KIPINDI CHA KUSOMA NA KUANDIKA' (DAKIKA 30)
Katika kuimarisha umahiri wa wanafunzi kujifunza kusoma na kuandika, ni muhimu mwalimu awe na mpango unaomwezesha kutumia maarifa mapya aliyojifunza wakati wa mafunzo ya walimu kazini kwa vitendo. Aidha, ni muhimu kwa wanafunzi kupata muda zaidi wa kujifunza kusoma na kuandika.

Kurasa zifuatazo zimesheheni mifano ya somo kazi wa jumla kwa ajili ya kazi mbili ambazo pamoja na mshirika mwingine unaweza kujaribu wakati wa vipindi vya kusoma na kuandika (au unaweza kujaribu wakati wa kipindi cha kawaida cha Kiswahili).

1. Soma kila mwongozo wa somo
2. Jaza nafasi zilizo wazi katika kila mwongozo wa somo
3. Halafu jaribu mikakati wakati wa kipindi cha kusoma na kuandika.

MWONGOZO WA SOMO NAMBA 1: Sauti ya Herufi

UMAHIRI MKUU: Ufahamu wa sauti za herufi

LENGO KUU: Mwanafunzi aelewe sauti za herufi

LENGO MAHSUSI: Mwanafunzi aweze kutofautisha sauti za herufi za mwanzo katika maneno

UMAHIRI MAHSUSI: Kutamka sauti za herufi katika maneno

ZANA ZA KUFUNDISHA: Orodha ya maneno

VITABU VYA REJEA: Moduli ya 6

MCHAKATO WA UFUNDISHAJI

HATUA	MUDA	VITENDO VYA UFUNDISHAJI	VITENDO VYA KUJIFUNZA
UTANGULIZI	**10**	Anza kipindi kwa zoezi la kuchangamsha kwa kutumia Mchezo ule ule wa kulala ambao uliutumia mwanzoni mwa moduli ya 6. Asili maelekezo hayo katika darasa lako	
MAARIFA MAPYA	**5**	Baada ya kucheza mchezo wa kulala, eleza kwamba maneno yanayotamkwa yameundwa na sauti tofauti. Mchezo wa kulala umetoa mifano ya maneno ambayo yanaonekana tofauti kwa sababu yanaanza na sauti tofauti, kama vile, 'maji' na 'nazi'	**Kusikiliza maelezo ya mwalimu kuhusu sauti za herufi**

KUPANGA MKAKATI

(Zunguka uangalie kama walimu wanahitaji msaada)

KUPANGA MKAKATI

HATUA	MUDA	VITENDO VYA UFUNDISHAJI	VITENDO VYA KUJIFUNZA
KUIMARISHA MAARIFA	**5**	1. Tumia mbinu ya 'Ninafanya – Tunafanya – Mnafanya' kufundisha sauti za herufi. 2. Kwanza, anza na 'Ninafanya': Tamka 'maji' taratibu sana. Waoneshe namna ya kusema neno taratibu sana. 3. Kisha, endelea na 'Tunafanya': Himiza darasa lifanye zoezi hilo kwa pamoja na wewe. Waambie wawe makini kuangalia namna midomo na ndimi zao vinavyobadilika wakati wanatamka sauti tofauti za herufi. Wakati mdomo unabadilika, wanatengeneza sauti tofauti ya herufi. 4. Mwisho, maliza na 'Mnafanya': Himiza wanafunzi waseme 'maji' taratibu sana wenyewe. 5. Kama wanafunzi wanashindwa kutambua sauti ya herufi inayoanza katika neno, wape mifano mingine na wairudie.	**Kuzingatia namna midomo na ndimi zao vinavyobadilika wakati wa kutamka sauti mbalimbali za maneno**
KUTUMIA MAARIFA	**10**	6. Fanya zoezi la kutambua sauti ya herufi kama hiyo katika maneno tofauti (kwa mfano, mama, meza, mtu, muda). Hii inawasaidia wanafunzi kusikia sauti hizo katika muktadha mbalimbali. 7. Baada ya kutamka maneno mbalimbali taratibu, uliza wanafunzi ni sauti gani wanayoisikia mwanzoni mwa kila neno. Sauti hiyo ni /m/ 8. Waambie watoe mifano mingine ya maneno yanayoanza na sauti /m/ 9. Baada ya wanafunzi kuweza kubainisha sauti ya herufi /m/, angalia orodha ya sauti ndefu za herufi na chagua herufi nyingine kutoka katika orodha hiyo. Fikiria maneno yanayoanza na herufi hiyo na rudia hatua ya 1-6 10. Baada ya kukamilisha sauti ndefu za maneno, endelea na sauti fupi za maneno.	**Kufanya mazoezi ya kutamka maneno taratibu** **Kuzingatia sauti tofauti katika neno** **Kubainisha sauti za mwanzo za maneno**
UPIMAJI	**10**	11. Waambie wanafunzi wafungue madaftari yao na waeleze kwamba utasoma maneno tofauti sita. (Kama unafundisha sauti ya herufi /m/, fikiria maneno matatu yanayoanza na sauti hiyo na matatu mengine yanayoanza na sauti nyingine ya herufi) 12. Waeleze wanafunzi kwamba, kama neno unalolisema linaanza na sauti /m/, wataandika alama ya (√) kwenye mstari. 13. Kama neno hilo halianzi na sauti /m/, wataandika alama ya "X" kwenye mstari. 14. Kama unafanya tathmini hii kwa mazungumzo tu, wanafunzi watainua tu mikono yao kama wanafikiri maneno yanaanza na sauti inayofanana. Kisha andika idadi ya wanafunzi waliojibu kwa usahihi. 15. Kama wanafunzi hawawezi kusikia tofauti kati ya sauti mbalimbali za herufi, rudia somo hilo kwa kutumia mifano mingine ya maneno	**Kubainisha sauti za mwanzo za herufi.**

Tathmini: _____

Maoni: _____

KUPANGA MKAKATI

(Zunguka uangalie kama walimu wanahitaji msaada)

KUPANGA MKAKATI

MWONGOZO WA SOMO NAMBA 2: Natafuta

UMAHIRI MKUU: Kubainisha sauti za herufi

LENGO KUU: Mwanafunzi afanye mazoezi ya kubainisha sauti za herufi

LENGO MAHSUSI: Mwanafunzi aweze kubaini mwanzo mwanzo wa sauti za herufi

UMAHIRI MAHSUSI: Kusikiliza sauti ya herufi ya mwanzo na kutamka neno sahihi

ZANA ZA KUFUNDISHA: Orodha ya maneno

VITABU VYA REJEA: Moduli ya 6

MCHAKATO WA UFUNDISHAJI

HATUA	MUDA	VITENDO VYA UFUNDISHAJI	VITENDO VYA KUJIFUNZA
UTANGULIZI	**10**	1. Kabla ya siku ya somo, kagua darasa na chagua vitu kadhaa vyakufanyia kazi. 2. Fikiri kuhusu sauti za mwanzo na mwishoni mwa vitu/ maneno hayo. 3. Waeleze wanafunzi kuwa watafanya kazi katika makundi. 4. Waambie wanafunzi kwamba utaanza kuangalia katika vitu vilivyoko karibu na darasa na kuwadokeza kidogo. Wao watapaswa kubashiri katika makundi yao kuhusu kitu ambacho unaongelea. 5. Wagawe wanafunzi kwenye makundi (wagawe kulingana na madawati ambayo wanakalia– kama una darasa kubwa, ligawe katika makundi mawili yakitengwa na usawa wa katikati ya chumba cha darasa).	**Kusikiliza maelekezo ya mwalimu kuhusu namna ya kucheza mchezo wa 'Natafuta'**
MAARIFA MAPYA	**5**	6. Sema "natafuta" kitu ambacho kiko ndani ya darasa kinachoanza na sauti, kwa mfano / d/. Halafu, elekeza kundi kutafuta kitu hicho ndani ya darasa ambacho kinaanza na sauti iliyosemwa. Makundi lazima yafikiri mara nyingi kadri yawezavyo. Mfano: Mwalimu anasema: Natafuta kitu kinachoanza na sauti /d/ Wanafunzi wanajadiliana na kuja na jibu, "dawati," "dirisha," "daftari," n.k.	**Kusikiliza maelezo ya mwalimu kuhusu mchezo wa 'Natafuta'**

KUPANGA MKAKATI

(Zunguka uangalie kama walimu wanahitaji msaada)

KUPANGA MKAKATI

MCHAKATO WA UFUNDISHAJI

HATUA	MUDA	VITENDO VYA UFUNDISHAJI	VITENDO VYA KUJIFUNZA
KUIMARISHA MAARIFA	**15**	7. Yapatie makundi dakika tano kujadiliana na yaruhusu yaseme orodha ya maneno ambayo wamepata. 8. Toa alama kwa kila neno sahihi watakalolisema. 9. Kundi lenye alama nyingi limeshinda. 10. Endelea na hatua 6-8 kwa kutumia vitu mbalimbali ulivyobainisha darasani kwako. 11. Karibisha wanafunzi 1 -2 kujitolea kulieleza darasa sauti inayoanza ya kitu ambacho unatafuta. Karibisha darasa zima kubashiri kitu hicho.	**Kubainisha sauti za mwanzo za maneno**
KUTUMIA MAARIFA	**10**	12. Unaweza kucheza mchezo huohuo lakini kwa kuanza na sauti fulani, kwa mfano unatafuta kitu kinachoanza na sauti fulani au unatafuta kitu ambacho kinaishia na sauti ya / a /. Kwa mfano, /a/ = dirisha, meza, ruba, n.k.	**Kubainisha sauti ya herufi ya mwisho katika maneno**
UPIMAJI	**5**	13) Kuangalia na kusikiliza wanafunzi wakicheza mchezo. Weka kumbukumbu ya wanafunzi ambao hawawezi kutambua sauti za herufi. Vilevile weka kumbukumbu ya sauti za herufi ambazo zinatatiza wanafunzi. Rudia kuzifundisha kwa kutumia andalio la somo lililopita.	**Kubainisha sauti ya herufi ya mwanzo na ya mwisho katika maneno**

Tathmini: _____

Maoni: _____

UFUATILIAJI

WAAMBIE WALIMU:

" Tunaendelea kusoma matini kwa sauti na kwa kupokezana."

UFUATILIAJI

UFUATILIAJI

Baada ya kujifunza moduli hii, mratibu elimu kata, afisa elimu wa wilaya, pamoja na wakaguzi watafuatilia kuona namnaunavyotumia ujuzi ulioupata katika ufundishaji wako darasani. Ni vizuri uwe tayari kwa ufuatiliaji huo kwa kuandaa:

- Eleza tofauti kati ya sauti ya herufi na jina la herufi
- Onesha kwa vitendo sauti za herufi zote katika alfabeti ya Kiswahili
- Taja majina ya herufi kwa kila herufi ya alfabeti ya Kiswahili (siyo alfabeti ya Kiingereza)
- Onesha kwa vitendo masomo mawili ambayo yanasaidia mwanafunzi aweze kubainisha mwanzo na mwisho wa sauti za herufi

MWISHO

WAAMBIE WALIMU:

""Walimu, tumefika mwisho wa moduli yetu, tumia dakika kumi kutafakari somo letu la leo. Jaza fomu kurekodi tathmini yako ya moduli. Baada ya kukamilisha chomoa ukurasa huo unipatie. Tafadhali uwe mkweli katika majibu yako kwa sababu yatasaidia kuboresha Mafunzo ya Walimu Kazini ngazi ya shule hapo baadaye."

Kusanya fomu za tathmini zilizokamilishwa na walimu na uwe nazo wakati wa mkutano mwingine katika kundi la kata.

Wakati walimu wanaendelea kujaza fomu za tathmini, tafadhali tafakari kwa ujumla juu ya mafanikio na changamoto zilizojitokeza katika kipindi cha siku hiyo na jaza visanduku vinavyofuata. Haya utaweza kuyajadili pamoja na Timu ya Wilaya ya Mafunzo Walimu Kazini na Waratibu wengine wa Mafunzo Walimu Kazini wa mkutano unaofuata katika kundi la kata.

MAFANIKO YA JUMLA YA KIPINDI HIKI:	CHANGAMOTO ZA JUMLA ZA KIPINDI HIKI:

Shule: _____ **Wilaya:** _____ **Mkoa:**_____

Tafakuri za Moduli # _____ **Mada ya Moduli:** _____

Idadi ya walimu walioshiriki : _____ **Mwalimu Mkuu alishiriki : Ndiyo/Hapana**

MWISHO

MWISHO (DAKIKA 10)

Binafsi jaza fomu ifuatayo kuweka rekodi ya tathmini ya moduli ya leo. Baada ya kukamilisha, chomoa ukurasa huu na umpe Mratibu wako. Tafadhali uwe mkweli kwa vile mrejesho wako utasaidia kuboresha Mafunzo ya Walimu Kazi ngazi ya shule hapo baadaye.

JEDWALI LA KUTATHMINI			
Alama 0: Sikubaliani kabisa na usemi huu	**Alama 1: Kwa kiasi Sikubaliani** na usemi huu	**Alama 2: Nakubaliana kwa kiasi** na usemi huu	**Alama 3: Nakubaliana Kabisa** na usemi huu

FOMU YA TATHMINI

Shule: _____ **Wilaya:** _____ **Mkoa:**_____

Tathmini ya Moduli: _____ **Mada ya Moduli:** _____

Idadi ya walimu walioshiriki: _____ **Mwalimu Mkuu alishiriki: Ndiyo/Hapana**

Mratibu alikuwepo kuwezesha: Ndiyo/Hapana

Soma semi zifuatazo kisha weka alama ya vema katika kisanduku husika kuonesha jibu lako:	**0**	**1**	**2**	**3**
1. Dhana kuu ya moduli ya leo ilikuwa inaeleweka.				
2. Moduli hii ina mikakati mingi mizuri na yenye manufaa ambayo nitaitumia darasani kwangu.				
3. Muda uliotumika kukamilisha moduli hii unafaa. Sikuhisi kwamba ni muda mrefu sana.				
4. Moduli hii iliibua mjadala wa kufurahisha na tafakuri ya hali ya juu sana.				
5. Violezo vya kipindi cha kusoma na kuandika vilisaidia sana. Natarajia vitakuwa rahisi kuvitumia ndani ya darasa langu.				
6. Zana tulizotengeneza leo zitakuwa za manufaa sana (kama inahusika).				
7. Mratibu amejiandaa kwa kipindi – amesoma vizuri moduli na ameandaa vifaa vyote vya kufundishia.				
8. Mratibu anasimamia vizuri majadiliano – anajua jinsi ya kuwafanya watu wajieleze na namna ya kupata majibu.				
9. Mratibu anajua namna ya kusimamia makundi – anahakikisha kuwa walimu wanatoa ushirikiano, wanashirikiana na wana hamasika.				
10. Mratibu anajua jinsi ya kuwahamasisha walimu – anafuatilia kujua waliokosa vipindi au kuchelewa na kutukumbusha kwanini Mafunzo ya Walimu Kazini ni muhimu kwetu.				